

Home > Ukweli Uliopotea – Sehemu ya Kwanza > Safari Yangu Kuelekea Madhehebu Ya Ahlul- Bayt > Hadiya

---

# Safari Yangu Kuelekea Madhehebu Ya Ahlul- Bayt

## Hadiya

Kwa aliyezaliwa kwenye ngome ya umaasumu na uchaMwenyezi Mungu, na mashukio ya wahyi na uongofu, na mrithishwa wa fadhila tukufu na ukarimu.

Imwende mwanamke mwema, na mpambanaji mtoa nasaha, aliye huru mkataaji, na ni muujiza Muhammadiyah, na ni hazina Haydaria, na ni amana Fatmiyah.

Imwende aliyekuwa mtii wa Mwenyezi Mungu, katika hali ya siri na ya wazi, na aliyetoa changamoto kwa msimamo wake dhidi ya wanafiki na wafitini.

Imwende aliyewatia hofu masultani wakorofi kwa msimamo wake thabiti, na alizishangaza akili kwa umadhubuti wa moyo wake, na alifanana na baba yake Ali kwa ushujaa wake, na alishabihiana na mama yake Zahra'a kwa utukufu wake na balagha yake.

Imwende aliye nasibika na ukoo wa kinabii na uimamu, aliyetunukiwa shani ya cheo, utukufu na karama. Imwende shujaa wa Karbalaa bibi wa kibani Hashim. *Sayyidatiy wa Maulatiy Zaynab (a.s.)*.

---

**Source URL:** <https://www.al-islam.org/node/25184>